SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

OFISI YA RAIS KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ILIYOWASILISHWA MBELE YA BARAZA LA WAWAKILISHI NA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI

MHE. SHARIFF ALI SHARIFF (MBM)

MEI 2025



**MHE. SHARIFF ALI SHARIFF (MBM)**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI ZANZIBAR.**

# YALIYOMO


**YALIYOMO**.......................................................................................i
VIFUPISHO VYA MANENO.......................................................................iii
A. UTANGULIZI ..................................................................................... 1
B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI .................................................................... 2
C. UTEKELEZAJI WA BAJETI WA OFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA - JULAI 2024 - MACHI 2025.............................................................................. 4
i. Mapato yaliyokusanywa kwa Fungu A07............................................ 4
ii. Muhtasari wa Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa Fungu AO7 ...................................................................... 4
iii. Muhtasari wa Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa Fungu A11. ....................................................................... 5
D. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI, 2024 - MACHI 2025......... 5
i. Utekelezaji wa Programu kwa Fungu A07.......................................... 5
Programu Kuu PA0702: Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote ...................................................................... 5
Programu Kuu PA0703: Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.................... 8
Programu Kuu PA0705: Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji......................................................................... 9
Programu Kuu PA0801: Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.................................................. 10
ii. Utekelezaji wa Programu kwa Fungu A11 ........................................... 13
Programu Kuu PA1101: Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi........................ 13
Programu Kuu PA1102: Uendeshaji na Utumishi wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar............................................... 15
E. MAELEZO KUHUSIANA NA BAJETI INAYOZINGATIA USAWA WA KIJINSIA YA OFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI (ORKUU) 16
F. CHANGAMOTO NA NJIA ZA UTATUZI ..................................................... 18
G. MUELEKEO WA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI KWA MWAKA 2025/2026 (BAJETI NA MAOMBI YA FEDHA) ........................................ 19

i. Vipaumbele vya Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji na Taasisi zake. .......... 19
ii. Shughuli zitakazofanyika kwa kila Programu kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 .......... 21
H. PROGRAMU KUU PA0702: USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA AJIRA ZA STAHA KWA WOTE. .......... 21
I. PROGRAMU KUU PA0703: UIMARISHAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA. 22
J. PROGRAMU KUU PA0704: KUIMARISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA BINAFSI .......... 23
K. PROGRAMU KUU PA0705: UENDESHAJI NA URATIBU WIZARA.......... 24
iii. Shughuli zitakazofanyika kwa kila Programu kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 - Fungu Nam 11.......... 25
L. PROGRAMU KUU PA1101: UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI .......... 25
M. PROGRAMU KUU PA1102: UENDESHAJI NA UTUMISHI WA WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI .......... 26
iv. Maombi ya Kuidhinishiwa Makadirio ya Mapato. .......... 26
v. Maombi ya Fedha za Makadirio ya Matumizi kwa Fungu A07 .......... 27
vi. Maombi ya Fedha kwa Makadirio ya Matumizi ya Fungu A11 (Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi).......... 27
vii. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa ZIPA .......... 28
N. SHUKRANI. .......... 28
VIAMBATISHO .......... 31

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| COSTECH | Commission For Science and Technology |
| CRDB | Cooperative and Rural Development Bank |
| FAO | Food and Agriculture Organisation |
| HRM | Human Resource Management |
| IOM | International Organization for Migration |
| ILO | International Labour Organisation |
| MBM | Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi |
| MTEF | Mid Term Expenditure Framework |
| NGOs | Non Governmental Organisations |
| ORKUU | Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji |
| PBZ | Peoples' Bank of Zanzibar |
| PDF | Project Development Fund |
| PPP | Public Private Partnership |
| SACCOS | Saving and Credit Cooperative Society |
| SJMT | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| SP | Strategic Plan |
| TCB | Tanzania Commercial Bank |
| TV | Television |
| TZS | Tanzania Shillings |
| UAE | United Arab Emirates |
| UNDP | United Nation Development Programmes |
| USD | United State Dollar |
| WIMS | Workplace Information Management System |
| ZADEP | Zanzibar Development Plan |
| ZANEMA | Zanzibar National Employment Association |
| ZATUC | Zanzibar Trade Union Congress |
| ZEEA | Zanzibar Economic Empowerment Agency |
| ZIPA | Zanzibar Investment Promotion Authority |
| ZSSF | Zanzibar Social Security Fund |

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na hatimae likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

2. **Mheshimiwa Spika,** Nianze hotuba yangu kwa Kumshukuru Allah (Subhanahu Wataala) kwa Rehma zake kutujaalia uhai, uzima wa afya na kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza hili kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

3. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuchukua fursa hii adhimu kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zao wanazozichukua za kudumisha amani, utulivu, mshikamano na kuleta maendeleo ya Taifa letu. Naomba kuwapongeza sana kwa Kuteuliwa na Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Kugombea nafasi ya Urais kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa Afya njema, uwezo na busara ya kuliongoza na kulitumikia Taifa hili.

4. **Mheshimiwa Spika,** Kwa heshma kubwa nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mafanikio makubwa alioyapata katika kusimamia Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Kitaifa. Katika uongozi wake wananchi wa Zanzibar wameshuhudia maendeleo makubwa katika ujenzi wa miundombinu ya Bararbara kubwa na za ndani, uimarishaji wa huduma za bandari na viwanja vya ndege, uimarishaji wa huduma za jamii ikiwemo ujenzi wa masoko ya kisasa, kuongezeka kwa fedha za uwezeshaji Wananchi kiuchumi, maskuli, hospitali na viwanja vya michezo na huduma nyengine

katika maeneo huru ya uwekezaji na kuimarisha uwekezaji katika visiwa vidogo vidogo.

5. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, nawapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Othman Masoud Othman - Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili wa Rais, pamoja na Mhandisi Zena Ahmed Said - Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais kutimiza azma na malengo yake ya kuiletea maendeleo Zanzibar na wananchi wake.

6. **Mheshimiwa Spika,** Vile vile, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, na Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza kwa kuendesha vikao vya Baraza la Wawakilishi kwa umahiri na uweledi mkubwa. Kipekee, namshukuru Mheshimiwa Mtumwa Peya Yussuf - Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya Baraza hili ikiwemo Ofisi yako na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo kwa mashirikiano makubwa wanayotupatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ikiwemo kupitia utekelezaji wa programu kwa kila robo mwaka na kufanya mapitio ya Bajeti hii ya mwaka 2025 – 2026. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa ushauri, maelekezo na michango yao wanayonipatia ambayo yamefanikisha utekelezaji wa majukumu niliyopangiwa.

7. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi, salaamu na pongezi, naomba sasa uniruhusu kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ikijumuisha Muundo na Majukumu ya Ofisi, Utekelezaji wa Programu, Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2024/2025, Mafanikio na Changamoto zilizojitokeza na utatuzi wake.

## B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

8. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Kibajeti inajumuisha Mafungu Makuu mawili (2) inayoundwa na

Idara saba (7), Taasisi mbili (2) na Ofisi Kuu Pemba. Malengo makuu ya kuanzishwa Ofisi hii ni kusimamia masuala kazi, uwekezaji na uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa kutekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Kukuza na kusimamia uwekezaji kwa maendeleo ya Nchi,

ii. Kuratibu fursa za ajira na kusimamia upatikanaji wa ajira za staha Nchini hasa katika sekta binafsi

iii. Kusimamia utekelezaji wa mikataba, sheria, kanuni na miongozo ya kazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa na kuimariasha mahusiano mazuri ya kazi miongoni mwa Serikali, Sekta Binafsi, waajiri na vyama vya wafanya kazi.

iv. Kuimarisha usalama na afya kazini,

v. Kukuza na kusimamia maendeleo ya vyama vya Ushirika,

vi. Kuimarisha na kukuza Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi,

vii. Kukuza na kuimarisha Miradi inayotekelezwa kwa mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi,

viii. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa Sera, Sheria, programu na tafiti zinazohusiana na masuala ya kazi, ajira, uwekezaji, uwezeshaji na miradi ya mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi,

ix. Kuimarisha utaratibu, mashirikiano, ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Ofisi pamoja na kuelimisha jamii juu ya shughuli za Ofisi kupitia mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano

x. Kusimamia na kuimarisha masuala ya utumishi na uendeshaji ikiwemo kuleta ufanisi wa kiutendaji na maslahi ya wafanyakazi.

## C. UTEKELEZAJI WA BAJETI WA OFISI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA - JULAI 2024 - MACHI 2025

9. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, umegawika katika maeneo makuu manne (4) kupitia mafungu mawili (Fungu A07 na A11) ambayo ni; Ukusanyaji wa Mapato, Matumizi ya Ofisi, Miradi ya Maendeleo na Utekelezaji wa Shughuli za Taasisi zilizo chini ya Ofisi.

### i. Mapato yaliyokusanywa kwa Fungu A07.

10. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Ofisi ilikadiriwa kukusanya Mapato ya TZS. 6,695,428,000. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2024/2025 imekusanya jumla ya TZS. 3,876,810,247 sawa na asilimia 78 kwa makadirio ya miezi tisa ya TZS 5,021,571,000. **Kiambatisho namba 1 kinafafanua.**

Aidha, Ofisi inatarajia kukusanya jumla ya TZS 5,426,673,847 hadi kufikia Juni 2025.

### ii. Muhtasari wa Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa Fungu AO7

11. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi kupitia Fungu A07 iliidhinishiwa Jumla ya Matumizi ya TZS. 28,326,400,000 ambapo mishahara ni TZS. 8,688,800,000, matumizi ya kawaida TZS.4,637,600,000 na miradi ya maendeleo TZS. 15,000,000,000. Katika kipindi cha Julai – Machi, Ofisi imeingiziwa Jumla ya TZS. 7,214,880,931 sawa na asilimia 33 ya makadirio ya matumizi ya miezi tisa (9). Kati ya fedha hizo mishahara ni TZS.5,566,022,291 sawa na asilimia 80, Matumizi ya Kawaida TZS. 1,648,858,640 sawa na asilimia 35.5 na hakuna fedha iliyoingizwa katika Mradi wa Maendeleo wa Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji - Fumba. **Kiambatisho namba 2a,2b,2c na 2d vinafafanua.**

**iii. Muhtasari wa Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa Fungu A11.**

12. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (Fungu A11) kwa mwaka wa fedha 2024/2025, iliidhinishiwa jumla ya matumizi ya TZS 46,879,700,000 ambapo mishahara ni TZS. 1,257,700,000 matumizi ya kawaida TZS. 2,022,000,000 na miradi ya maendeleo ya TZS. 43,600,000,000.

Hadi kufikia Machi, 2025 Wakala imeingiziwa Jumla ya TZS. 1,625,080,801 sawa na asilimia 5 ya makadirio ya bajeti kwa miezi 9. Kati ya fedha hizo mishahara ni TZS. 1,012,795,870 sawa na asilimia 107, Matumizi ya Kawaida TZS. 612,284,931 sawa na asilimia 37 na hakuna fedha iliyoingizwa katika miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Khalifa na INUKA. **Kiambatisho namba 3a, 3b,3c, na 3d vinafafanua.**

## D. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI, 2024 - MACHI 2025

### i. Utekelezaji wa Programu kwa Fungu A07

**Programu Kuu PA0702: Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote**

13. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina programu ndogo tatu ambazo ni Programu ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha; Programu ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini na Programu ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini.

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu iliidhinishiwa Matumizi ya TZS. 2,178,000,000 na hadi kufikia Machi, 2025 imepatiwa TZS. 1,441,928,945 sawa na asilimia 66 .

14. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025, imetekeleza shughuli zifuatazo;

1. Imeratibu upatikanaji wa ajira za ndani 8,366 (wanaume 5,089 na wanawake 3,277) katika kazi za hospitali, hoteli, vituo vya mafuta na skuli. Kwa upande wa ajira za nje ya nchi kupitia Mawakala Binafsi wa Ajira jumla ya Vijana 5,830 (wanaume 815 na wanawake 5,035) wamepatiwa Ajira katika Nchi za Oman, Kuwait, Qatar, Saudia-Arabia na UAE kwa kazi za Vibarua, Udereva, Hoteli na kazi za Majumbani. Ajira hizi ni sawa na asilimia 77 ya lengo la mwaka la uratibu wa upatikanaji wa ajira za ndani na nje 18,500 iliojiwekea Idara. Hivyo, katika miaka minne (4) upatikanaji wa ajira umefikia 233,615 (sekta rasmi 157,789 na sekta isiyo rasmi 75,827) sawa na asilimia 78 ya lengo iliyojiwekea katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025 ya ajira 300,000. Kati ya ajira hizo wanaume 116,476 sawa na asilimi 49.8 na wanawake 117,139 sawa na asilimia 50 zikiwemo ajira za nje 10,580 (wanaume 1,804 na wanawake 8,776).

2. Imetoa mafunzo kwa vijana 50 ya ufundi wa simu kupitia programu maalum ya kukuza ujuzi kwa vijana wasio na ajira, elimu na hawapo katika mafunzo yoyote (NEET Program) katika Chuo cha Karume. Vijana hawa ni sawa na asilimia 50 ya lengo la vijana 110 waliopatiwa mafunzo ya kukuza ujuzi.

3. Imetayarisha Mfumo wa watafuta kazi (Job Seekers Portal) kwa watafuta kazi pamoja na kutoa mafunzo kwa wadau wa ajira (mawakala na watafuta kazi) ili waweze kutumia mfumo huo.

4. Imetoa elimu ya masuala ya kazi, ajira, usalama na afya kazini na umuhimu wa Vyama vya Wafanyakazi kupitia vipindi vya redio, makongamano, warsha na kufika katika maeneo ya kazi.

5. Imesajili sehemu za kazi 175 (122 Unguja na 53 Pemba) na kukagua sehemu za kazi 273 (188 Unguja na 85 Pemba) Kati ya usajili wa sehemu za kazi 160 na ukaguzi wa maeneo ya kazi 240 yaliyopangwa kwa mwaka. Pia, imetoa mafunzo kwa wafanyakazi 1,503 kutoka Taasisi za umma 22 na Taasisi binafsi 14 kwa lengo la kuangalia masuala ya usalama na afya katika sehemu za kazi.

6. Imeandaa Rasimu za Kanuni tatu (Kanuni kiongozi, kanuni ya huduma ya kwanza kazini na kanuni ya kutoa taarifa kwa matukio ya ajali na maradhi yatokanayo na kazi kwa ajili ya kufafanua Sheria ya Usalama na Afya kazini nambari 8 ya mwaka 2005.

7. Imesimamia viwango vya kazi kwa wazawa kwa kuthibitisha mikataba ya kazi 9,713 (8,491 na Pemba 1,222) sawa na asilimia 194 ya makadirio ya mikataba 5,000 ya mwaka kwa lengo la kuhakikisha masharti na viwango vya mikataba vinaendana na sheria, kanuni na miongozo ya kazi iliopo nchini.

8. Imefanya ukaguzi kazi katika sehemu za kazi 324 (Unguja 229 na Pemba 95) ili kusimamia na kulinda haki na maslahi ya wafanyakazi ambayo ni sawa na asilimia 54 ya lengo la ukaguzi kazi 600 kwa mwaka.

9. Imepokea migogoro ya kazi 296 kati ya hiyo, migogoro 170 imetatuliwa sawa na asilimia 104 ya lengo la kutatua migogoro 162 kwa mwaka. Aidha, migogoro 126 inaendelea kufanyiwa kazi ili kuimarisha mahusiano mema kazini pamoja na kuimarisha utekelezaji wa sheria za kazi. Migogoro hiyo inahusu kuachishwa kazi, madai ya mishahara, madai ya likizo, malipo ya skukuu za kitaifa, muda wa ziada na kutokupewa mikataba.

10. Imeandaa Mfumo wa malipo (Billing Management System) kwa ajili ya kuimarisha malipo ya vibali vya kazi kwa wageni. Aidha, imetoa vibali 1,395 kwa wataalamu wa kigeni vyenye thamani ya TZS.2,582,034,397/=.

11. Imewajengea uwezo watendaji 22 (Unguja 15 na Pemba 7) wa taaluma ya kutumia mfumo wa ukaguzi wa maeneo ya kazi (Strategy Compliance Planning System) kwa kushirikiana na ILO. Aidha, imetoa mafunzo ya usuluhishi na uamuzi wa migogoro kwa kutumia mfumo wa kidigitali ili kuongeza ufanisi.

12. Imefanya vikao 5 vya kuimarisha ushirikiano wa Vyama vya Wafanyakazi, Waajiri na Serikali pamoja na kutatua Migogoro mitano (5) ya vyama vya wafanyakazi ili kuimarisha mahusiano mema kazini.

Migogoro hiyo inahusu ada za Wanachama, kutoka Uanachama na Migogoro ya Viongozi ndani ya Chama,

13. Imefanya ukaguzi wa vyama 5 na Matawi 7 ya Vyama vya Wafanyakazi na Jumuiya za waajiri kupitia Sheria ya Mahusiano Kazini namba 1 ya mwaka 2005 ili kuhakikisha vyama hivyo vinafuata sheria na katiba zao.

14. Imefanya matayarisho ya kuanzisha programu za mafunzo ya masuala ya kazi na mahusiano kazini (labour relations training program) kwa kufanya mkutano na wadau wa masuala ya kazi.

15. Imeandaa Mpango wa tatu wa Nchi wa Kazi za Staha (Decent Work Country Program III ) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu ya Tanzania Bara, ILO, Washirika wa utatu (ZATUC, ZANEMA, ATE, TUCTA) na Wadau wengine.

16. Imetekeleza sheria ya ajira namba 11 ya mwaka 2005 katika kupambana na ajira za Watoto kwa kukagua maeneo yanayotumikishwa Watoto yakiwemo masoko, madiko, bandari na kuanzisha madawati kwa kuzuia ajira za watoto kwa kushirikiana na ILO.

**Programu Kuu PA0703: Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.**

**15. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina programu ndogo moja ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika.

Programu hii iliidhinishiwa matumizi ya TZS. 1,080,725,000 na hadi kufikia Machi, 2025 ilipatiwa TZS. 408,231,508 sawa na asilimia 38.

**16. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025, imetekeleza shughuli zifuatazo;

1. Imesajili vyama vya Ushirika 1,352 (735 Unguja na 617 Pemba) sawa na asilimia 75 ya lengo la kusajili vyama 1,800 kwa mwaka na kufanya ukaguzi wa hesabu wa vyama vya Ushirika 211 (106

Unguja na 105 Pemba) pamoja na kufanya ufuatiliaji na uchunguzi wa vyama vya ushirika 444 (149 Unguja na 295 Pemba).

2. Imefanya utafiti wa mageuzi ya vyama vya Ushirika kwa lengo la kufanya mageuzi katika usajili wa vyama vya ushirika kidigitali, kuangalia fursa zilizopo za kuendeleza vyama vya ushirika kisasa, kupata taarifa za vyama vya ushirika kwa wakati na popote na kutoa elimu za kifedha, kibiashara na kimasoko ili vyama kupata tija ya kutoa ajira, kukuza mitaji na kuongeza ujuzi.

3. Imefanya matayarisho ya awali ya Mfumo wa Kielektroniki ya Usajili na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika kwa kufanya pia majadiliano na Tume ya Maendeleo ya Ushirika ya Tanzania Bara.

4. Imetoa mafunzo kwa vyama vya Ushirika 1,812 (570 Unguja na 1,242 Pemba) sawa na asilimia 79 ya lengo la vyama 2,300 kwa mwaka kwa washiriki 8,837 (Wanawake 6,940 na Wanaume 1,897) ili kujenga uelewa juu ya dhana ya Ushirika, Uwekaji wa kumbukumbu za hesabu, ujasiriamali, masoko, mabadiliko ya mtazamo na kujitambua.

**Programu Kuu PA0705: Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.**

17. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina programu ndogo tatu ambazo ni Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Ofisi, Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji na Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi Pemba.

Programu hii iliidhinishiwa matumizi ya TZS. 5,659,806,600 na hadi kufikia Machi, 2025 imepatiwa TZS. 2,461,826,482 sawa na asilimia 43.

18. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, programu imetekeleza shughuli zifuatazo;

1. Imekamilisha utafiti wa taarifa za ajira kwa sekta rasmi na sekta isiyo rasmi ambapo matokeo yameonesha katika miaka minne (4)

upatikanaji wa ajira umefikia ajira 233,615 (sekta rasmi 157,789 na sekta isiyo rasmi 75,827).

2. Imefanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Wizara (SP) kwa lengo la kupima utekelezaji wa mipango ya Wizara. Aidha, imefanya mapitio ya Agenda ya utafiti ya Wizara (research agenda) ili kurahisisha ufanyaji wa tafiti.

3. Imekamilisha Sera ya Uwekezaji na Sera ya Ajira na zipo katika hatua ya kuwasilishwa Serikalini.

4. Imeratibu vikao vya mashirikiano vya kitaifa kati ya Ofisi na Wizara za SJMT kwa Sekta ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Ushirika, Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi (PPP) pamoja na Kazi, Ajira, Afya na usalama kazini.

5. Imewapatia wafanyakazi 256 stahiki zao ikiwemo malipo ya mishahara na maposho mengineyo na posho la likizo kwa wafanyakazi 55.

6. Imeimarisha matumizi ya mifumo ikiwemo e- office, HRM Payroll na mfumo wa asset register.

7. Imetoa mafunzo ya muda mrefu kwa watendaji 14 (wanawake 9 na wanaume 5) na muda mfupi kwa Wafanyakazi 39 (wanawake 23 na wanaume 16) katika fani ya sheria, manunuzi na ugavi, Uchumi na fedha. Mafunzo ya muda mfupi katika fani ya Habari, kumbukumbu na nyaraka, ukatibu, Udereva,Tehama, na uandaaji wa Mpango Mkakati (SP)

8. Imeratibu uandaji wa Ripoti zikiwemo; ripoti za utekelezaji wa Bajeti, Ilani, matayarisho ya MTEF na Uandaaji wa Hotuba ya Bajeti.

**Programu Kuu PA0801: Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.**

**19. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina programu ndogo mbili ambazo ni Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji.

Programu hii iliidhinishiwa matumizi ya TZS. 4,407,868,400 na hadi kufikia Machi, 2025 ilipatiwa TZS. 2,902,893,996 sawa na asilimia 65

20. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025, imetekeleza shughuli zifuatazo;

1. Imepitisha Sheria mpya ya Uwekezaji namba 10 ya mwaka 2023 ambayo imeweka mazingira mazuri kwa Uwekezaji na Wawekezaji Nchini. Serikali pia imeimarisha huduma jumuishi za mfumo wa kielekroniki kwa kupunguza muda katika uidhinishaji wa maombi, utoaji wa vyeti vya uwekezaji na upatikanaji wa vibali vya kazi na ukaazi kwa wawekezaji. Hatua hizo zimepelekea kuongezeka kwa idadi ya miradi ambapo hadi kufikia Machi 2025, jumla ya miradi 480 imesajiliwa yenye thamani ya zaidi ya Dola 5.9 billion na kuzalisha ajira 18,000 nchini.

   Uwekezaji huu umejumuisha Uwekezaji mpya wa visiwa vidogo vidogo utakowekeza zaidi ya Dola za kimarekani 384.5 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, visiwa 20 vimetangazwa na 17 vimekodishwa, ambapo visiwa (Bawe, Pemunda A+B, Chapwani, Pungume, Kwata, Mnemba na Changu) tayari vimeshaanza ujenzi. Uwekezaji katika kisiwa cha Bawe umeshakamilika na kuanza kutoa huduma ambapo kimewekeza jumla ya Dola 42 milioni kwa ujenzi wa Hoteli ya nyota 5 kutoa ajira zipatazo 400 mradi huo unazalisha maji ya matumizi ya ndani kutoka maji ya bahari kwa na inatumia umeme wa jua unaozalishwa hapo hapo kisiwani kwa matumizi yake ya kila siku.

2. Kwa mwaka 2024/2025 Imesajili miradi ya uwekezaji Binafsi 70 sawa na asilimia 63.6 ya kusajili miradi 110 yenye thamani ya dola za kimarekani 330,740,134 inayotarajiwa kutoa ajira 1,467 kwa wananchi. Miradi hiyo ni katika Sekta ya hoteli, nyumba za makazi ( Real Estate) na Viwanda pamoja na kukagua miradi 73 mipya inayohitaji kuekezwa na kutoa vibali vya ujenzi vipatavyo 34.

   Aidha, miradi 10 imefunguliwa na kuanza kutoa huduma ikiwemo Miradi ya hoteli na Nyumba za Makaazi.

3. Imekamilisha utiaji saini wa Mkataba kwa ujenzi wa barabara ya kilomita 8 katika eneo la Fumba pamoja na kuendelea na matayarisho ya kufanya tathmini na uhakiki wa wananchi watakaopatiwa fidia kupisha ujenzi wa barabara hizo.

4. Imekamilisha utafiti na kutoa ripoti ya mwenendo wa mitaji binafsi kutoka kwa wageni (Private capital flow survey) mzuguko wa 15 na ripoti ya mzunguko wa 16 imeanza kutayarishwa.

5. Imeshiriki na kufanya Makongamano ya kimataifa kuhusiana na Biashara na Uwekezaji katika Nchi za Korea, China, UAE, Indonesia, Oman na Saudi Arabia, Dar-es-Salam na Zanzibar.

6. Imekamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa Kukuza Uwekezaji Zanzibar.

7. Serikali ya awamu ya nane mnamo mwaka 2021 imefanya mageuzi makubwa katika kushajihisha uwekezaji wa miradi ya Mashirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi (Public Private Partnership – PPP), yakiwemo kuunda Wizara maalum inayosimamia Uwekezaji, kufanya marekebisho ya Sheria ya PPP kuruhusu miradi kuasisiwa na Wawekezaji (Unsolicited Projects) kuunda Timu ya Mashauriano ya Serikali (Government nigotiation team- GNT) pamoja na kuruhusu miradi hiyo kwenda katika majidiliano ya moja kwa moja ili kurahisisha utekelezaji.

   Hatua hizo zimepelekea kuengezeka kwa idadi ya miradi ya PPP na hati kufikia Machi 2025, jumla ya Miredi 18 ya mashirikiano imeshasainiwa na kuingia Mikataba. Miradi iliyokamilika na kuanza kutoa huduma ni Ujenzi na Uendeshaji wa Bandari ya Fumba, Uwendeshaji wa Jengo la Abiria (Terminal 3 ) katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA, Uwendeshaji wa Bandari ya Malindi na Bandari Kavu ya Maruhubi, Ukarabati na Uendeshaji wa Bandari ya Mkoani ambapo Mheshimiwa Rais alipokea Meli ya Mizigo pamoja na Ujenzi wa Bandari ya Abiria na Mizigo (Ro-Ro) Mpigaduri, (Ujenzi unaendelea).

Kwa mwaka 2024/2025 imepokea na kufanya uchambuzi wa miradi 29 ya mashirikiano, Kati ya hiyo, miradi 7 imepitishwa kwa kusainiwa mikataba ambayo ni Ujenzi wa Kituo cha Ushushaji wa Mafuta na Gesi (Mangapwani), Uendeshaji wa Uwanja wa Amani (New Amani Complex), Uimarishaji na Uendeshaji wa Karakana kuu ya Magari Zanzibar, Ujenzi wa Mifumo na Vituo vya Afya Zanzibar, Usambazaji wa Maji Zanzibar, Uendeshaji wa Soko na Diko la Malindi na Ujenzi na Uendeshaji wa Eneo la Biashara Jozani.

8. Imetoa elimu juu ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) kwa mawizara yakiwemo; Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi; Wizara ya Maji, Nishati na Madini; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ZSSF, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na Tume ya Mipango ili kuweza kubuni na kuandaa miradi ya mashirikiano (PPP).

9. Imefanya mapitio ya Sheria na imetayarisha kanuni, miongozo, Models, na nyenzo (Tools) za uwezeshaji wa miradi ya PPP.

**ii. Utekelezaji wa Programu kwa Fungu A11.**

**Programu Kuu PA1101: Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.**

**21. Mheshimiwa Spika;** Programu hii ina programu ndogo moja ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Programu hii iliidhinishiwa matumizi ya TZS. 44,167,125,000 (567,125,000 kwa kazi za kawaida, na TZS 43,600,000,000 kwa programu za maendeleo) hadi kufikia Machi, 2025 ilipatiwa TZS. 193,569,838 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 34 kwa makadirio ya mwaka. Kwa upande wa programu za maendeleo hakuna fedha zilizoingizwa hadi kufikia Machi.

**22. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025, imetekeleza shughuli zifuatazo;

1. Imetoa taaluma kwa Mamlaka kumi na moja (11) za Serikali za mitaa kuhusiana na taratibu za mikopo. Aidha jumla ya TZS.

523,175,400.18 (Unguja TZS. 380,927,918.88 na Pemba TZS.142,247,481.30) zimepokelewa ambazo ni asilimia 10% za mapato ya ndani kupitia programu ya makundi maalum ya 4:4:2. Kiambatisho namba 4 kinafafanua

2. Imetoa mikopo yenye thamani ya TZS. 6,616,166,637.03 (Unguja TZS.4,916,878,000 na Pemba TZS. 1,699,288,637.03) kwa wananchi 2,661 ambapo Unguja 1,692 (wanawake 1,135 na wanaume 557) na Pemba 969 ambapo (wanawake 673 na wanaume 296) kati ya wananchi 26,000 kwa programu za vifaa vya nyuki, Inuka, Khalifa na 4:4:2. Lengo hili halikufikiwa kutokana kwa kukosekana kwa fedha za maendeleo. Kiambatisho namba 5 kinafafanua

3. Imepokea Jumla ya fedha TZS. 8,332,497,371.86 za marejesho ya mikopo ambapo Unguja ni TZS.5,966,394,983.14 na Pemba ni TZS.2,366,102,388.72 . Kiambatisho namba 6 kinafafanua

4. Imetoa Mafunzo kwa wajasiriamali 3,098 ambapo kwa Unguja 2696 (wanaume 550 na wanawake 2,146) na Pemba 402 (wanaume 200 na wanawake 202) sawa na asilimia 65 ya lengo la wajasiriamali 4,750 kwa mwaka. Mafunzo hayo ni katika fani ya ujasiriamali, ufugaji nyuki, mpango wa biashara, usarifu wa matunda na mbogamboga, umeme wa jua, masuala ya fedha na masoko. **Kiambatisho namba 7 kinafafanua**

5. Imeunganisha Wajasiriamali 363. Unguja 305 (wanaume 89, na wanawake 216), na Pemba 58 (wanaume 19, na wanawake 39) zaidi ya lengo la wajasiriamali 210 kwa mwaka katika fursa za masoko kupitia Tamasha la fahari ya Zanzibar, maonesho ya jua kali, maonesho ya Mapinduzi Tamasha la Kizimkazi.

6. Imeunganisha Wajasiriamali 38 (Unguja 17 na Pemba 21) na Taasisi ya ubora na viwango kwa ajili ya kuwaombea alama ya ubora ili waweze kuendana na mahitaji ya soko na ushindani wa kibiashara kati ya Wajasiriamali 60 kwa mwaka.

7. Imetoa huduma za kiufundi na Ushauri wakitalamu kwa viwanda 132 (Unguja 24, na Pemba 108) katika masuala ya mashine, mitambo na utumiaji wa kemikali zaidi ya lengo la viwanda 50 kwa mwaka.

8. Imeandaa program maalum ya kukuza ujasiriamali katika vyuo vikuu ambayo inalenga kusaidia kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana nchini ili kuwezesha kujiajiri.

**Programu Kuu PA1102: Uendeshaji na Utumishi wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar.**

**23. Mheshimiwa Spika;** Programu hii ina programu ndogo mbili ya Utumishi na Uendeshaji na Ofisi ya Uratibu wa Wakala Pemba na kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilikadiriwa TZS. 2,712,575,000. (TZS 1,454,875,000 kwa kazi za kawaida, na TZS. 1,257,700,000 kwa kwa ajili ya Mishahara) Hadi kufikia Machi, 2025 imepatiwa matumizi ya TZS. 1,431,510,962 (TZS. 418,715,093 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 29, na TZS. 1,012,795,870 kwa ajili ya mshahara sawa na asilimia 81.

**24. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, programu hii ilijipangia kutoa mafunzo na kuboresh maslahi ya wafanyakazi, kuimarisha huduma za uendeshaji na Utawala na kuratibu masuala ya uwezeshaji nchini,kufanya ufatiliaji na tathmini na kuimarisha mashirikiano ya kitaifa. Programu hii imetekeleza mambo yafuatayo:

1. Imewajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi watendaji 10 katika fani za ukaguzi, vihatarishi na usimamizi wa manunuzi, utunzaji wa kumbukumbu na uandishi wa ripoti.

2. Imewapatia wafanyakazi 104 stahiki za mishahara na posho zinazoendana na mishahara, Aidha imeimarisha maslahi ya wafanyakazi 32 (Unguja 21, na Pemba 11) kwa kuwapatia maposho mengineyo yakiwemo maposho ya likizo, malipo ya muda wa ziada, nyongeza ya mshahara, na kusaidia gharama za mazishi. Aidha, imepitisha muundo wa Taasisi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi.

3. Imefanya ufuatiliaji kwa wanufaika 182 katika huduma za Uwezeshaji ili kuangalia mahitaji yao ikiwemo alama ya ubora, umeme, vifungashio na miundombinu.

4. Imetayarisha mifumo 3 (mikopo, mafunzo na masoko) ili kurahisisha utoaji huduma pamoja na kutoa vipindi 28 vya Redio na TV

5. Imeshiriki katika makongamano yanayohusu masuala ya Uwezeshaji yakiwemo siku ya wanawake, jukwaa la bajeti na uchumi kwa ajili ya wajasiriamali.

6. Imetayarisha mifumo mitatu ya kielektroniki ( mfumo wa mikopo, mafunzo na masoko) kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma.

7. Kwa upande wa Pemba, imeratibu upatikanaji wa huduma mbali mbali kwa wajasiriamali 142 zikiwemo ushauri wa kibiashara, uombaji wa mikopo na taratibu za kuomba alama za ubora.

## E. UZINGATIAJI WA USAWA WA KIJINSIA KATIKA BAJETI

**25. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ina jukumu la kuinua hali ya kijamii na kiuchumi ya wananchi wa Zanzibar kupitia utoaji na upatikanaji wa fursa za kiuchumi zilizopo, kuhamasisha utamaduni na uwezo wa ujasiriamali, kusaidia maendeleo ya viwanda vidogo na vya kati, kukuza na kusimamia uwekezaji kwa maendeleo ya Nchi, upatikanaji wa ajira zenye staha na uzingatiaji wa sheria na viwango vya kazi.

**26. Mheshimiwa Spika,** Katika kufikia dhamira hii, maeneo ya kuzingatia ya kijinsia ni; uwepo wa watoto chini ya umri wa miaka 18 katika ajira za kutumikishwa; kuwepo kwa Vijana ambao hawajapata elimu, hawapo katika ajira na hawajapatiwa mafunzo ya aina yeyote; baadhi ya watu wenye ulemavu wanashindwa kukidhi masharti ya Kikundi kwa ajili ya kusajili ili waweze kupatiwa mkopo; ushiriki mdogo wa wanaume katika mafunzo yanayotolewa na Kituo cha kulea na kukuza wajasiriamali (ZTBI) ukilinganisha na wanawake

kutokana na aina ya bidhaa zinazofundishwa kama vile uokaji, usindikaji wa matunda na mbogamboga; bidhaa zinazozalishwa na vijana kukosa alama ya ubora na baadhi ya kaya katika maeneo ya Vijijini haziwezi kumudu gharama za kuunganishiwa umeme wa gridi ya Taifa.

Katika kuzingatia masuala ya Jinsia, kwa mwaka wa fedha 2025/26 ORKUU imetenga rasilimali zake kwa shughuli zifuatazo;

a) Kuwaondoa watoto chini ya umri wa miaka 18 katika ajira za kutumikishwa; watoto 68 wameondolea kwenye utumikishwaji kwa mwaka 2024/2025 na Watoto 100 ndio shabaha mwaka 2025/2026;

b) Kuratibu na kuwezesha programu ya Mafunzo kazi kwa Vijana (NEET) kulingana na mahitaji; kutoka vijana 50 kwa mwaka 2024/25 na vijana 70 kwa mwaka 2025/26.

c) Kuratibu na kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa watu wenye ulemavu kupitia programu ya 4:4:2; Kwa mwaka 2024/2025 watu wenye ulemavu 228 wamepatiwa mikopo na mwaka 2025/2026 inalenga kuwapatia mikopo watu wenye ulemavu 30.

d) Kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana juu ya ufugaji wa nyuki na usindikaji wa asali; kwa mwaka 2024/25, wanaume 536 walipata mafunzo na kwa mwaka 2025/26 inalenga kuwapatia mafunzo wanaume 1,000.

e) Kuwaunganisha wajasiriamali na wazalishaji kujisajili bidhaa zao katika taasisi za usajili na viwango; Kwa mwaka 2024/2025 wajasiriamali 38 wameunganishwa na alama za ubora na mwaka 2025/2026 inalenga kuwaunganisha wajasiriamali 90.

f) Kuwawezesha wanawake kushiriki katika mafunzo ya ufungaji wa vifaa vya umeme wa jua kwa kaya za vijijini.kwa mwaka 2024/25, wanawake 21 walipatiwa mafunzo hayo na kwa mwaka 2025/26 inalenga kuwapatia wanawake 25.

Kwa mwaka wa fedha 2025/26, jumla ya bajeti ya TZS. 233,320,000/= imetengwa kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na TZS. 2,377,830,000/= kutoka kwa Wadau wa Maendeleo ili kutekeleza shughuli hizo.

## F. CHANGAMOTO NA NJIA ZA UTATUZI

27. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio yaliyofikiwa Katika Utekelezaji wa bajeti ya Ofisi kwa mwaka 2024/2025 kupitia Idara na Taasisi zake tofauti pia kulikua na changamoto zifuatazo;

1. Kukosekana kwa mifumo ya kieletroniki katika kurahisisha utendaji kazi ili kuweza kutoa huduma bora.

   Ofisi imeshaanza matayarisho ya awali ya kukusanya taarifa zote zinazohitajika kwa ajili ya kuziwasilisha kwa mtaalamu elekezi ili aweze kujua mahitaji ya mfumo unaotakiwa.

2. Kukosekana kwa Fedha katika mfuko wa maendeleo ya miradi (PDF) kwa miradi ya PPP kwa ajili ya kutayarisha pembuzi yakinifu za miradi (Bankable projects) ya kisekta na fedha za matumizi ya kawaida na fedha za maendeleo ambazo zimeathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

   Katika kutatua changamoto hii, Mamlaka za utekelezaji (Sekta) zitenge bajeti maalumu kwa ajili ya kuandaa upembuzi yakinifu za miradi ya kisekta, pamoja na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuingiza fedha kulingana na mpangokazi.

3. Kutokupokea fedha za mchango wa asilimia 10 (4:4:2) kwa wakati kwa baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, na kutopokea kabisa fedha hizo kwa Wilaya ya Mjini.

   Ofisi kwa kushirikiana na ZEEA wanaendelea kufuatilia kwa karibu na kufanya majadiliano na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhusu upatikanaji wa fedha za asilimia 10 kutoka Mamlaka zote za Serikali za Mitaa.

4. Upungufu wa vitendea kazi vya Usalama na Afya Kazini, wafanyakazi na wataalamu katika Idara/taasisi kwa fani za uhandisi, afya, mahusiano kazini, ukaguzi kwa Unguja na Pemba.

   Kuwasilisha mahitaji ya wafanyakazi na wataalamu kwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora pamoja na kuomba wafanyakazi kutoka Taasisi nyengine za Serikali.

5. Wananchi kukosa mikopo kutokana na Kutoingiziwa kwa fedha za Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2024/2025 iliyotarajiwa kuingizwa TZS. 43,600,000,000. Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kujipanga kuwasilisha fedha za mikopo kama maombi yalivyowasilishwa ili kuwawezesha wananchi.

## G. MUELEKEO WA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI KWA MWAKA 2025/2026 (BAJETI NA MAOMBI YA FEDHA)

**28. Mheshimiwa Spika,** matayarisho ya bajeti hii yamezingatia Dira ya Maendeleo ya mwaka 2050, Mpango Mkakati wa Maendeleo (ZADEP), Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025 na Maagizo ya Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mpango mkakati wa Ofisi ya Rais kazi Uchumi na Uwekezaji.

**29. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi itaendelea kusimamia upatikanaji wa ajira kwa vijana, kusimamia sheria za kazi pamoja kuimarisha uwekezaji na uwezeshaji ili kuimarisha uchumi wa nchi na ustawi wa jamii yetu. Malengo hayo yataendelea kutekelezwa kupitia Programu Kuu Sita (6) kupitia Mafungu Mawili ambayo ni Fungu A07 (Kazi, Uchumi na Uwekezaji) na Fungu A11 (Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

### i. Vipaumbele vya Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji na Taasisi zake.

**30. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi imejipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

1. Kuratibu upatikanaji wa Ajira za staha, kuimarisha mazingira ya kazi na mahusiano kazini, kusimamia ulinzi wa haki za

Wafanyakazi, ulinzi wa afya na usalama kazini na utatuzi wa migogoro ya kazi na kufanya Mageuzi ya Kitaasisi ili kuimarisha utendaji kazi.

2. Kuimarisha Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi 20,000, kuwezesha vikundi vya kijamii, kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kukuza masoko ya bidhaa.

3. Kufanya mageuzi ya Vyama vya Ushirika kwa kushajihisha matumizi ya mifumo ya kidigitali katika usimamizi na ufatiliaji wa shughuli, kuimarisha upatakinaji wa masoko kupitia ushirikiano na ndani na nje ya nchi, kuweka mifumo madhubuti ya ukaguzi na usimamizi wa fedha, kuhimiza uwazi, maadili na uwajibikaji pamoja na kujenga uwelewa kuhusu misingi ya ushirika yenye tija.

4. Kukuza na kuwezesha Uwekezaji Binafsi kwa kuimarisha mazingira ya uwekezaji, mifumo rafiki ya Tehama, miundombinu ya uwekezaji katika maeneo huru, na kurahisisha taratibu za utoaji huduma (One-Stop Center) ili kushajihisha uwekezaji wenye tija zaidi wa kimkakati na uwekezaji katika visiwa vidogo vidogo.

5. Kushajihisha Uwekezaji wa Mashirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi katika miradi ya kimkakati ya Nishati (Energy), Utalii wa Daraja Binafsi la juu (Tourism and Hospitality), Teknolojia (ICT), Uchumi wa Buluu, Anga (Aviation), “Maritime and Industrial facililty”, Afya na Huduma za Jamii (Healthcare and Public Services) na Michezo (Sports and Recreation).

31. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa vipaumbele vilivyotajwa vitakwenda sambamba na uimarishaji wa Sera, Sheria, Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini na Tafiti, pamoja na kuimarisha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wa Ofisi ili kuleta ufanisi.

ii. **Shughuli zitakazofanyika kwa kila Programu kwa mwaka wa Fedha 2025/2026**

## H. PROGRAMU KUU PA0702: USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA AJIRA ZA STAHA KWA WOTE.

32. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo;

1. Kuratibu upatikanaji wa ajira za staha 4,000 nje ya Nchi na Ajira 16,000 ndani ya Nchi.

2. Kusimamia utekelezaji wa programu za ukuzaji ujuzi kwa vijana 70.

3. Kuandaa vitini vya mafunzo kwa wasafiri wafanyakazi nje ya Nchi.

4. Kufanya ukaguzi kazi kwa taasisi binafsi 708 Unguja na Pemba na ukaguzi wa vyama vya wafanyakazi 13 na jumuia za waajiri 2 kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji wa sheria za kazi na mahusiano kazini zinafuatwa.

5. Kutoa vibali vya kazi kidigitali kwa wataalamu wa kigeni wanaokuja kufanya kazi Nchini.

6. Kupambana na ajira za watoto katika sehemu za kazi kwa ajili ya kuzuia utumikishwaji wa Watoto chini ya miaka 18.

7. Kusuluhisha na kuamua migogoro inayohusiana na masuala ya kazi na vyama vya wafanyakazi.

8. Kuthibitisha mikataba ya kazi 10,500 kwa ajili ya kuhakikisha mikataba hiyo inakidhi viwango vya kimataifa.

9. Kuridhia mikataba sita ya Shirika la Kazi Duniani inayohusiana na usalama na afya kazini, hifadhi ya jamii, mafao ya wafanyakazi wanaopata majanga kazini, wafanyakazi wa majumbani, sera ya ajira na mfumo wa uhamasishaji wa masuala ya usalama na afya kazini.

10. Kufanya mapitio ya sheria za kazi ili ziendane na wakati uliopo.
11. Kufanya utafiti wa kuanzisha programu za mafunzo ya kazi na mahusiano kazini (labour relations training program).
12. Kukamilisha mfumo wa usimamizi wa taarifa za kazi kidijitali (comprehensive labour management system).
13. Kukuza na kuimarisha mashirikiano ya UTATU baina ya Serikali, vyama vya wafanyakazi na jumuia ya waajiri ili kuondosha changamoto za ajira.
14. Kukagua sehemu za kazi 240 na kusajili sehemu za kazi 120 kwa lengo la kulinda usalama na afya kazini.
15. Kuandaa mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa usalama na afya kazini Workplace Information Management System (WIMS).
16. Kusimamia Sheria ya usalama na afya kazini na kuandaa kanuni 5 zinazohusiana na masuala ya usalama na afya kazini.
17. Kushiriki mikutano na makongamano ya Kitaifa na Kimataifa yanayohusiana na masuala ya kazi, ajira na usalama na afya kazini.
18. Kutoa elimu kwa waajiri, waajiriwa na jamii katika masuala ya kazi, vyama vya wafanyakazi, ajira na usalama na afya kazini.

## I. PROGRAMU KUU PA0703: UIMARISHAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA.

**33. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo;

1. Kusajili vyama vya ushirika 2000, kukagua vyama 500 na kufuatilia vyama vya ushirika 1000.
2. Kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni za maendeleo ya vyama vya Ushirika.

3. Kuandaa mfumo wa usajili wa Vyama vya Ushirika kidijitali ili kuweza kuvifuatilia, kuvisimamia na kutoa mafunzo yanayohitajika yakiwemo biashara, masoko, usimamizi ya fedha na ukaguzi kwa ufanisi.

4. Kuimarisha mashirikiano na wadau wakuu wa sekta ya ushirika na kushiriki mikutano ya kitaifa na kimataifa.

## J. PROGRAMU KUU PA0704: KUKUZA NA KUIMARISHA UWEKEZAJI NCHINI

**34. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo;

1. Kufanya mapitio ya maandiko ya miradi mipya 22 ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi.

2. Kusaidia na kuwezesha miradi ya PPP 20 iliyopitishwa kwa ajili ya utekelezaji.

3. Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi 15 ya PPP kwa lengo la kutathmini utekelezaji wake.

4. Kusajili miradi ya uwekezaji 90 yenye thamani ya USD 390,670,000 na inayotarajiwa kutoa ajira kwa wazawa zipatazo 3,000.

5. Kushiriki na kuandaa mikutano, makongamano na maonesho ya Kitaifa na Kimataifa kwa lengo la kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini.

6. Kuendeleza ujenzi wa miundombinu katika maeneo huru ya uwekezaji.

7. Kufanya utafiti wa mwenendo wa mitaji binafsi kwa miradi ya wageni awamu ya 17 na kutoa ripoti ya mwaka ya mwenendo wa uwekezaji nchini.

8. Kusimamia utekelezaji wa miradi ya uwekezaji katika visiwa vidogo vidogo.

9. Kuandaa Mpango Mkakati wa Uenezi na Masoko, Mpango Mkakati wa Mahitaji na Matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki na Mpango Mkakati wa Biashara na Uwekezaji kwa Taasisi.

10. Kuandaa Mfumo wa Utambuzi wa Ardhi na Miradi ya Uwekezaji (Land Maping System) na kukamilisha uundaji wa Mfumo wa Kutoa Huduma kwa Wawekezaji awamu ya tatu (Zanzibar Investment Electronic Window phase three).

11. Kuimarisha huduma za Ofisi za uwekezaji ikiwemo mifumo ya kielektroniki, utoaji wa mafunzo na upatikanaji wa vifaa vya Ofisi.

12. Kuendelea na Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya ZIPA eneo la Mbweni Matrekta pamoja na kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi ya ZIPA Pemba.

13. Kuandaa Mpango wa Matumizi wa eneo la Shamba la RAZABA lenye ukubwa wa hekta 6,000 lililopo Bagamoyo kwa ajili ya Uwekezaji.

14. Kuanza Ujenzi wa Mtaa wa Viwanda katika maeneo ya Micheweni Pemba.

## K. PROGRAMU KUU PA0705: UENDESHAJI NA URATIBU WA OFISI

**35. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo;

1. Kuratibu utekelezaji wa mipango, programu na miradi ya Ofisi na kuandaa Mpango Mkakati (SP) wa Wizara.

2. Kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Ushirika.

3. Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini pamoja na upatikanaji wa takwimu za Ofisi na kufanya Mpango wa utekelezaji wa Agenda ya Utafiti.

4. Kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

5. Kuimarisha utendaji wa wafanyakazi 30 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na wafanyakazi 3 mafunzo ya muda mrefu.

6. Kuwezesha safari za kikazi Ndani na Nje ya Nchi.

7. Kuimarisha huduma za uendeshaji za Ofisi ikiwemo Ununuzi wa Vifaa, matengenezo ya Ofisi, habari na mawasiliano na ulinzi na huduma nyengine za ofisi.

8. Kuendelea kutumia na kuimarisha mifumo ya Ofisi ikiwemo e-office, Assets Register na Mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu (Human Resource Management).

9. Kuratibu shughuli za Ofisi Pemba kwa kusimamia utekelezaji wa masuala ya kazi na ajira, utatuzi wa migogoro ya kazi, ushirika, usalama na afya kazini uwekezaji, utumishi, uwendeshaji na mipango ya Ofisi

**iii. Shughuli zitakazofanyika kwa kila Programu kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 - Fungu Nam 11**

**L. PROGRAMU KUU PA1101: UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

**36. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo;

1. Kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi 20,000 (Unguja 12,000 na Pemba 8,000)

2. Kuwaunganisha wajasiriamali na wazalishaji 90 (Unguja 60 na Pemba 30) kwa ajili ya kuwapatia alama za ubora katika Taasisi ya Viwango

3. Kutoa mafunzo ya Uwezeshaji kulingana na mahitaji ya wananchi 4300 (Unguja 3500 na Pemba 800)

4. Kutoa taaluma kwa masheha na mamlaka za Serikali za Mitaa 11 (Unguja 7 na Pemba 4) kuhusu uwezeshaji

5. Kuwaunganisha wajasiriamali, wazalishaji na wafanya biashara 392 (unguja 312 na Pemba 80) na fursa ya masoko.

6. Kutayarisha module za utoaji wa mafunzo ya Uwezeshaji.

**M. PROGRAMU KUU PA1102: UENDESHAJI NA UTUMISHI WA WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

**37. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina programu mbili ya Utumishi na Uendeshaji na Ofisi ya Uratibu wa Wakala Pemba. Kwa mwaka 2025/2026, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo;

1. Kutayarisha Mpango Mkakati wa Wakala wa Uwezeshaji wananchi kiuchumi.

2. Kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi kwa watendaji 28 pamoja na kulipa stahiki zao.

3. Kutayarisha muongozo na nyenzo za vihatarishi (Risk management framework and Tools).

4. Kuelimisha jamii katika masuala ya Uwezeshaji kupitia vyombo vya habari na mtandao wa kijamii

5. Kufanya ufuatiliaji na tathmini na kuimarisha takwimu za Ofisi Pemba.

6. Kufanya ufuatiliaji na Tathmini kwa wanufaika 400 wa huduma za Uwezeshaji.

**iv. Maombi ya Kuidhinishiwa Makadirio ya Mapato.**

**38. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026 inaomba idhini ya kukusanya jumla ya TZS. 7,209,087,725 kupitia vianzio vyake sita (6) ambavyo ni Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira za ndani na Nje ya Nchi, Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi, Ada za Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika.

### v. Maombi ya Fedha za Makadirio ya Matumizi kwa Fungu A07

**39. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji inaomba kuidhinishiwa makadirio ya matumizi ya jumla ya TZS. 28,700,300,000/= Kati ya fedha hizo TZS. 7,815,700,000/= ni Mishahara; TZS. 5,884,600,000 /= ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida; TZS. 15,000,000,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika programu kuu zifuatazo;

a. Programu kuu ya Usimamizi wa Sheria za kazi, ukaguzi kazi na kazi za staha kwa wote imekadiriwa matumizi ya TZS.2,819,300,000/=

b. Programu kuu ya Uwezeshaji wananchi Kiuchumi (Vyama vya Ushirika) imekadiriwa matumizi ya TZS.821,442,000/=

c. Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji imekadiriwa matumizi nya TZS.5,278,912,000/=

d. Programu kuu ya kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi imekadiriwa matumizi ya TZS.19,780,646,000/= Kiambatanisho nambari 8 Kinafafanua.

### vi. Maombi ya Fedha kwa Makadirio ya Matumizi ya Fungu A11 (Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi)

**40. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi (ORKUU) inaomba kuidhinishiwa makadirio ya matumizi yatayosimamiwa na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi jumla ya TZS. 14,656,600,000 /= Kati ya fedha hizo TZS. 1,733,400,000/= ni Mishahara; TZS. 2,323,200,000 /= ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida; TZS. 10,600,000,000 /= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika programu kuu zifuatazo;

i. Programu kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imekadiriwa matumizi ya TZS. 11,064,500,000/=

ii. Programu kuu ya Uendeshaji na Utumishi imekadiriwa matumizi nya TZS. 3,592,100,000/= Kiambatanisho nambari 9 Kinafafanua

**vii. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa ZIPA**

**41. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2025/2026 inatarajia kukusanya jumla ya TZS 3,830,790,616 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato na kutumia TZS. 3,800,000,000 kwa lengo la kushajihisha na kuwezesha uwekezaji nchini, kuimarisha miundombinu ya uwekezaji pamoja kusimamisha uendeshaji wa Taasisi.

## N. SHUKRANI.

**42. Mheshimiwa Spika;** Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji inatanguliza shukurani zake za dhati kwa mashirikiano mazuri kupitia taasisi tunazofanya kazi nao pamoja zikiwemo Taasisi za Serikali, Wakuu wa Mikoa, Wakuu Wa Wilaya na Jamii kwa ujumla. Kwa namna ya pekee Ofisi inawashukuru Washirika wa Maendeleo wakiwemo ILO, UNDP, FAO, IOM, Benki ya Dunia (World Bank) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Aidha, inazishukuru taasisi za kiraia zikiwemo ZATUC, ZANEMA, COSTECH, Chuo cha Ushirika Moshi, Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Mawakala Binafsi wa Ajira, Zanzibar Maisha Bora Foundation, Milele Foundation na Taasisi zote zinazoshirikiana nasi kwani si rahisi kuzitaja moja moja. Ofisi pia inazishukuru Benki ya PBZ, TCB, BOT, CRDB, SACCOS, Polisi, Uhamiaji, Ustawi wa Jamii na Sekretarieti ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binaadamu. Vile vile tunawaomba wadau wengine kujitokeza kusaidia uendelezaji wa Sekta za Kazi na Ajira, Uwezeshaji na Uwekezaji.

**43. Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuanzia Katibu Mkuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Ofisa Mdhamini Pemba; Wakurugenzi wa Taasisi na Idara, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi zilizopo chini ya Ofisi, wakuu wa vitengo na Wafanyakazi wote kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi.

44. **Mheshimiwa Spika;** Namshukuru kwa dhati Mke wangu na Wanafamilia yangu kwa ushirikiano, uvumilivu na uelewa mnaonionesha katika kutekeleza majukumu niliyopewa ya kazi. Mchango wenu umekuwa chachu muhimu ya kunipa utulivu, moyo na ari ya kuendelea kutekeleza majukumu kwa ufanisi na kuwajibika ipasavyo katika nafasi niliyopewa. Nathamini sana namna mnavyoelewa ugumu wa kazi yangu na mnavyoniwezesha kupata utulivu wa akili kazini, na hasa kwa mchango wenu wa kipekee katika kunitia moyo wakati wa changamoto. Bila mshikamamo,uvumilivu na maombi yenu mambo mengi yasingewezakana.

45. **Mheshimiwa Spika;** Kwa unyenyekevu na heshima kubwa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia sekta kuu za kiuchumi za Kazi na Ajira, Uwezeshaji na Uwekezaji. Ninampongeza kwa uongozi wake Madhubuti wenye hekima na juhudi zisizochoka katika kuwaletea maendeleo, amani na ustawi wananchi wa Zanzibar.

    Kupitia maono yake thabiti na sera zenye mwelekeo wa kuimarisha uchumi, ustawi wa jamii na usawa wa maendeleo katika kila sekta, tumeshuhudia mafanikio makubwa ambayo yanagusa maisha ya watu wetu kwa njia chanya. Naahidi nitafanya kazi kwa uadilifu na moyo wa kujitolea na kuendelea kumpa ushirikiano na kuunga mkono jitihada zake ili kuifikisha nchi yetu katika mafanikio makubwa zaidi.

46. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Nakishukuru sana Chama Changu, Chama cha Mapinduzi (CCM), Viongozi na Wanachama wote kwa kuniamini na kunipa ushirikiano wa dhati na moyo wa mshikamano ulionisaidia kuweza kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 kwa kishindo. Nawashukuru Ahsanteni sana.

47. **Mheshimiwa Spika;** Mwisho nawashukuru tena Wajumbe wa Baraza lako na nawaomba kuipokea, kujadili na hatimae kuikubali taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 na kuidhinisha makadirio ya Mapato jumla ya TZS. 7,209,087,725

na matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya jumla ya TZS 42,456,800,000 ili kufanikisha malengo tuliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

48. **Mheshimiwa Spika;** Naomba kutoa hoja.

**MHESHIMIWA. SHARIFF ALI SHARIFF (MBM)**
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI ZANZIBAR.**

# VIAMBATISHO

**Kiambatisho nambari. 1.**

## MUHTASARI WA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

| NAMBA YA KASMA | IDARA | VYANZO VYA MAPATO | MAKADIRIO YA MWAKA | MAKADIRIO MIEZI 9 | MAKUSANYO HALISI MIEZI 9 | % YA MAPATO | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1422012 | KAMISHENI YA KAZI | ADA YA UHAKIKI WA MIKATABA | 388,100,000 | 280,100,000 | 513,512,000 | 183% | Kuongezeka kwa Taasisi za kigeni na kuelimika kwa waajiri kujua umuhimu wa mikataba ya kazi kwa wafanyakazi wao. |
| 1422071 | IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI | ADA YA UKAGUZI WA USALAMA NA AFYA MAENEO YA KAZI | 1,000,000,000 | 751,000,000 | 270,552,000 | 36% | Upungufu wa wafanyakazi na vitendea kazi kwa Idara ya OSH |
| 1422075 | IDARA YA AJIRA | ADA YA UHAKIKI WA MIKATABA | 245,000,000 | 186,000,000 | 293,481,200 | 158% | Uwepo wa dawati la ajira na ongezeko la wasafiri nje ya nchi |

| NAMBA YA KASMA | IDARA | VYANZO VYA MAPATO | MAKADIRIO YA MWAKA | MAKADIRIO MIEZI 9 | MAKUSANYO HALISI MIEZI 9 | % YA MAPATO | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1422036 | IDARA YA MARNDELEO YA VYAMA VYA USHIRIKA | ADA YA USAJILI WA VYAMA VYA USHIRIKA | 100,000,000 | 120,300,000 | 22,430,000 | 19% | Usajili unatokana na uhitaji wa wananchi. |
| 1422037 | IDARA YA MARNDELEO YA VYAMA VYA USHIRIKA | ADA YA UKAGUZI WA VYAMA VYA USHIRIKA | 150,000,000 | 79,950,000 | 20,378,300 | 25% | upungufu wa wafanyakazi wa ukaguzi kutokana na kustaafu na uhamisho wa ndani |
| 1422011 | KAMISHENI YA KAZI | ADA YA VIBALI VYA KAZI KWA WAGENI | 4,484,129,000 | 3,211,214,764.92 | 2,582,034,397 | 80% | |
| | **JUMLA NDOGO UNGUJA** | | **6,367,229,000** | **4,628,564,764.92** | **3,702,387,897** | **83.5 %** | |
| 1422012 | KAMISHENI YA KAZI | ADA YA UHAKIKI WA MIKATABA | 12,000,000 | 7,860,000 | 6,153,000 | 78% | |
| 1422071 | IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI | ADA YA UKAGUZI WA USALAMA NA AFYA | 226,199,000 | 164,149,000 | 139,482,600 | 85% | Uhaba wa vitendea kazi kwa wafanyakazi wa kigeni |

| NAMBA YA KASMA | IDARA | VYANZO VYA MAPATO | MAKADIRIO YA MWAKA | MAKADIRIO MIEZI 9 | MAKUSANYO HALISI MIEZI 9 | % YA MAPATO | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MAENEO YA KAZI | | | | | |
| 1422036 | IDARA YA MARNDELEO YA VYAMA VYA USHIRIKA | ADA YA USAJILI WA VYAMA VYA USHIRIKA | 50,000,000 | 36,500,000 | 22,010,000 | 60% | Usajili unatokana na uhitaji wa wananchi. |
| 1422037 | IDARA YA MARNDELEO YA VYAMA VYA USHIRIKA | ADA YA UKAGUZI WA VYAMA VYA USHIRIKA | 40,000,000 | 30,300,000 | 6,776,750 | 22% | upungufu wa wafanyakazi wa ukaguzi kutokana na kustaafu na uhamisho wa ndani |
| | **JUMLA NDOGO PEMBA** | | **328,199,000** | **238,809,000** | **174,422,350** | **73%** | |
| | **JUMLA** | | **6,695,428,000** | **4,867,373,764.92** | **3,876,810,247** | **80%** | |

**Kiambatisho nambari. 2a**

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 (FUNGU A07)

| PROGRAMU | JUMLA YA BAJETI MWAKA (OC + SALARY+DEV.) 2024/2025 | JUMLA YA MAKADIRIO YA OC NA MSHAHARA +DEV JULAI-MACHI 2024/2025 | JUMLA YA MATUMIZI YA OC NA MSHAHARA JULAI-MACHI 2024/2025 | % YA MAKADIRIO JULAI - MACHI 2024/2025 | % YA BAJETI YA MWAKA 2024/2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| **PA0702 PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI** | **2,178,000,000** | **1,396,745,800** | **1,441,928,945** | **103** | **66** |
| Kamisheni ya kazi | 1,670,980,000 | 1,082,525,800 | 1,199,547,918 | 111 | 72 |
| Idara ya Usalama na Afya Kazini | 247,020,000 | 151,830,000 | 105,952,237 | 70 | 43 |
| Idara ya Ajira | 260,000,000 | 162,390,000 | 136,428,790 | 84 | 52 |
| **2. PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI** | **1,080,725,000** | **711,078,750** | **408,231,508** | **57** | **38** |
| Idara ya Maendeleo | 1,080,725,000 | 711,078,750 | 408,231,508 | 57 | 38 |

| PROGRAMU | JUMLA YA BAJETI MWAKA (OC + SALARY+DEV.) 2024/2025 | JUMLA YA MAKADIRIO YA OC NA MSHAHARA +DEV JULAI-MACHI 2024/2025 | JUMLA YA MATUMIZI YA OC NA MSHAHARA JULAI-MACHI 2024/2025 | % YA MAKADIRIO JULAI - MACHI 2024/2025 | % YA BAJETI YA MWAKA 2024/2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| ya Ushirika | | | | | |
| **3. PROGRAMU KUU YA KUSHAJIHISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA ZA UMMA NA SEKTA BINAFSI** | **19,407,868,400** | **14,490,613,800** | **2,902,893,996** | **20** | **15** |
| Maendeleo ya uimarishaji wa maeneo huru ya uwekezaji | 18,645,800,000 | 13,984,350,000 | 2,631,218,576 | 19 | 14 |
| Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi | 762,068,400 | 506,263,800 | 271,675,420 | 54 | 36 |
| **4. PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA** | **5,659,806,600** | **5,368,676,883** | **2,461,826,482** | **46** | **43** |
| Idara ya mipango sera na Utafiti | 1,039,737,600 | 882,705,700 | 348,750,592 | 40 | 34 |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 3,146,416,000 | 2,353,085,500 | 1,244,378,903 | 53 | 40 |
| Afisi Kuu Pemba | 1,473,653,000 | 2,132,885,683 | 868,696,987 | 41 | 59 |
| **JUMLA KUU** | **28,326,400,000** | **21,967,115,233** | **7,214,880,931** | **33** | **25** |

**Kiambatisho nambari. 2b**

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI YA OC KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 (FUNGU A07)

| PROGRAMU | BAJETI YA OC MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO YA OC JULAI-MACHI a2024/2025 | MATUMIZI HALISI YA OC JULAI-MACHI 2024/2025 | % YA MAKADIRIO JULAI - MACHI 2024/2025 | % YA BAJETI YA MWAKA 2024/2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| **1. PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI** | **848,800,000** | **534,286,000** | **523,081,263** | **98** | **62** |
| Kamisheni ya kazi | 341,780,000 | 220,066,000 | 280,700,236 | **128** | **82** |
| Idara ya Usalama na Afya Kazini | 247,020,000 | 151,830,000 | 105,952,237 | **70** | **43** |
| Idara ya Ajira | 260,000,000 | 162,390,000 | 136,428,790 | **84** | **52** |
| **2. PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI** | **615,200,000** | **361,935,000** | **140,942,389** | **39** | **23** |
| Idara ya Maendeleo ya Ushirika | 615,200,000 | 361,935,000 | 140,942,389 | **39** | **23** |
| **3. PROGRAMU KUU YA KUSHAJIHISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA ZA UMMA NA SEKTA BINAFSI** | **634,830,000** | **410,835,000** | **108,975,445** | **27** | **17** |
| Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi | 634,830,000 | 410,835,000 | 108,975,445 | **27** | **17** |

| PROGRAMU | BAJETI YA OC MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO YA OC JULAI-MACHI a2024/2025 | MATUMIZI HALISI YA OC JULAI-MACHI 2024/2025 | % YA MAKADIRIO JULAI - MACHI 2024/2025 | % YA BAJETI YA MWAKA 2024/2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| **3. PROGRAMU KUU YA KUSHAJIHISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA ZA UMMA NA SEKTA BINAFSI** | **634,830,000** | **410,835,000** | **108,975,445** | **27** | **17** |
| Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi | 634,830,000 | 410,835,000 | 108,975,445 | **27** | **17** |
| **4. PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA** | **2,538,770,000** | **2,485,641,750** | **875,859,543** | **35** | **34** |
| Idara ya mipango sera na Utafiti | 712,480,000 | 637,262,500 | 160,261,692 | **25** | **22** |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 1,122,590,000 | 835,216,000 | 352,054,974 | **42** | **31** |
| Afisi Kuu Pemba | 703,700,000 | 1,013,163,250 | 363,542,877.00 | **36** | **52** |
| **JUMLA KUU** | **4,637,600,000** | **3,792,697,750** | **1,648,858,640** | **43** | **36** |

**Kiambatisho nambari. 2c**

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI YA MISHAHARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 (FUNGU A07)

| PROGRAMU | BAJETI YA MSHAHARA MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO YA MSHAHARA JULAI-MACHI 2024/2025 | MATUMIZI HALISI YA MSHAHARA JULAI-MACHI | % YA MAKADIRIO JULAI - MACHI 2024/2025 | % YA BAJETI YA MWAKA 2024/2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| **1. PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI** | **1,329,200,000** | **862,459,800** | **918,847,682** | **107** | **69** |
| Kamisheni ya kazi | 1,329,200,000 | 862,459,800 | 918,847,682 | **107** | **69** |
| **2. PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI** | **465,525,000** | **349,143,750** | **267,289,119** | **77** | **57** |
| Idara ya Maendeleo ya Ushirika | 465,525,000 | 349,143,750 | 267,289,119 | **77** | **57** |
| **3. PROGRAMU KUU YA KUSHAJIHISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA ZA UMMA NA SEKTA BINAFSI** | **3,773,038,400** | **2,829,778,800** | **2,793,918,551** | **99** | **74** |

| PROGRAMU | BAJETI YA MSHAHARA MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO YA MSHAHARA JULAI-MACHI 2024/2025 | MATUMIZI HALISI YA MSHAHARA JULAI-MACHI | % YA MAKADIRIO JULAI - MACHI 2024/2025 | % YA BAJETI YA MWAKA 2024/2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Maendeleo ya uimarishaji wa maeneo huru ya uwekezaji | 3,645,800,000 | 2,734,350,000 | 2,631,218,576 | **96** | **72** |
| Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi | 127,238,400 | 95,428,800 | 162,699,975 | **170** | **128** |
| **4. PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA** | **3,121,036,600** | **2,883,035,133** | **1,585,966,939** | **55** | **51** |
| Idara ya mipango sera na Utafiti | 327,257,600 | 245,443,200 | 188,488,900 | **77** | **58** |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 2,023,826,000 | 1,517,869,500 | 892,323,929 | **59** | **44** |
| Afisi Kuu Pemba | 769,953,000 | 1,119,722,433 | 505,154,110 | **45** | **66** |
| **JUMLA KUU** | **8,688,800,000** | **6,924,417,483** | **5,566,022,291** | **80** | **64** |

**Kiambatisho nambari. 2d**

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI YA FEDHA ZA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 (FUNGU A07)

| PROGRAMU | BAJETI YA MAENDELEO YA MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO YA MAENDELEO (JULAI 2024 - MACHI, 2025) | MATUMIZI YA MAENDELEO, (JULAI 2024 - MACHI, 2025) | %YA MAKADIRIO (JULAI 2024 - MACHI, 2025) | %YA BAJETI YA MWAKA (JULAI 2024 - MACHI, 2025) |
|---|---|---|---|---|---|
| **3. PROGRAMU KUU YA KUSHAJIHISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA ZA UMMA NA SEKTA BINAFSI** | **15,000,000,000** | **15,000,000,000** | **0** | **0** | **0** |
| Maendeleo ya uimarishaji wa maeneo huru ya uwekezaji | 15,000,000,000 | 15,000,000,000 | 0 | 0 | **0** |
| **JUMLA KUU** | **15,000,000,000** | **15,000,000,000** | **0** | **0** | **0** |

**Kiambatisho nambari. 3a**

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 (FUNGU A11)

| PROGRAMU | BAJETI YA MWAKA (OC+SALARY +DEV) 2024/2025 | JUMLA YA MAKADIRIO YA OC , MSHAHARA +DEV (JULAI 2024 - MACHI, 2025) | JUMLA YA MATUMIZI YA OC, MISHAHARA NA DEV (JULAI 2024 - MACHI, 2025) | %YA MAKADIRIO (JULAI 2024 - MACHI, 2025) | %YA BAJETI YA MWAKA (JULAI 2024 - MACHI, 2025) |
|---|---|---|---|---|---|
| **PA1101: Programu kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi** | **44,167,125,000** | **33,203,978,000** | **193,569,838** | **1** | **0.4** |
| SA110101: Programu ndogo ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 44,167,125,000 | 33,203,978,000 | **193,569,838** | 0.6 | 0.4 |
| **PA1102: Programu Kuu ya Utumishi na Uendeshaji wa Taasisi ya ZEEA** | **2,712,575,000** | **2,074,108,500** | **1,431,510,962** | **69** | **53** |
| SA110201: Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji | 1,985,217,000 | 1,526,295,500 | **1,076,024,241** | 70 | 54 |
| SA110202:Programu ndogo ya Afisi ya Uratibu - Pemba | 727,358,000 | 547,813,000 | **355,486,721** | 65 | 49 |
| **JUMLA KUU** | **46,879,700,000** | **35,278,086,500** | **1,625,080,801** | **5** | **3** |

**Kiambatisho nambari. 3b**

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI YA OC KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 (FUNGU A11)

| MAELEZO | BAJETI YA OC YA MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO YA OC , (JULAI 2024 - MACHI, 2025) | MATUMIZI YA OC, (JULAI 2024 - MACHI, | %YA MAKADIRIO (JULAI 2024 - MACHI, 2025) | %YA BAJETI YA MWAKA (JULAI 2024 - MACHI, 2025) |
|---|---|---|---|---|---|
| **PA1101: Programu kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi** | **567,125,000** | **503,978,000** | **193,569,838** | **38** | **34** |
| SA110101: Programu ndogo ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 567,125,000 | 503,978,000 | 193,569,838 | 38 | 34 |
| **PA1102: Programu Kuu ya Utumishi na Uendeshaji wa Taasisi ya ZEEA** | **1,454,875,000** | **1,130,833,500** | **418,715,093** | **37** | **29** |
| SA110201: Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji | 955,275,000 | 753,839,000 | 277,100,493 | 37 | 29 |
| SA110202:Programu ndogo ya Afisi ya Uratibu - Pemba | 499,600,000 | 376,994,500 | 141,614,600 | 38 | 28 |
| **JUMLA KUU** | **2,022,000,000** | **1,634,811,500** | **612,284,931** | **37** | **30** |

**Kiambatisho nambari. 3c**

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI YA MISHAHARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 (FUNGU A11)

| MAELEZO | BAJETI YA MSHAHARA YA MWAKA | MAKADIRIO YA MSHAHARA (JULAI 2024 - | MATUMIZI YA MSHAHARA, (JULAI 2024 - | %YA MAKADIRIO (JULAI 2024 - MACHI, 2025) | %YA BAJETI YA MWAKA (JULAI 2024 - MACHI, 2025) |
|---|---|---|---|---|---|
| **PA1101: Programu kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi** | - | - | - | - | - |
| SA110101: Programu ndogo ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **PA1102: Programu Kuu ya Utumishi na Uendeshaji wa Taasisi ya ZEEA** | **1,257,700,000** | **943,275,000** | **1,012,795,870** | **107** | **81** |
| SA110201: Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji | 1,029,942,000 | 772,456,500 | 798,923,749 | 103 | 78 |
| SA110202:Programu ndogo ya Afisi ya Uratibu - Pemba | 227,758,000 | 170,818,500 | 213,872,121 | 125 | 94 |
| **JUMLA KUU** | **1,257,700,000** | **943,275,000** | **1,012,795,870** | **107** | **81** |

**Kiambatisho nambari. 3d**

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI YA FEDHA ZA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 (FUNGU A11)

| PROGRAMU | BAJETI YA MAENDELEO YA MWAKA 2024/2025 (TZS) | MAKADIRIO YA MAENDELEO (JULAI 2024 - MACHI, 2025) (TZS) | MATUMIZI YA MAENDELEO, (JULAI 2024 - MACHI, 2025) | %YA MAKADIRIO (JULAI 2024 - MACHI, 2025) | %YA BAJETI YAMWAKA (JULAI 2024 - MACHI, 2025) |
|---|---|---|---|---|---|
| **PA1101: Programu kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi** | **43,600,000,000** | **32,700,000,000** | **0** | **0** | **0** |
| SA110101: Programu ndogo ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 43,600,000,000 | 32,700,000,000 | 0 | 0 | **0** |
| **JUMLA KUU** | **43,600,000,000** | **32,700,000,000** | **0** | **0** | **0** |

**Kiambatanisho nambari 4**

## MAKUSANYO YA MABARAZA/HALMSHAURI ZOTE JULAI 2024 – MACHI 2025

| BARAZA/HALMASHAURI | MAKADIRIO | FEDHA ILIYOKUSANYWA | % |
|---|---|---|---|
| MJINI | 276,650,500.00 | 0 | - |
| MAGHARIBI "A" | 155,327,825.30 | 60,000,000 | 39% |
| MAGHARIBI "B" | 199,550,194.50 | 13,651,687.20 | 7% |
| KASKAZINI "A" | 190,404,275.00 | 59,857,844.00 | 31% |
| KASKAZINI "B" | 133,306,500.00 | 78,893,288.20 | 59% |
| KATI | 120,207,665.20 | 101,403,731.53 | 84% |
| KUSINI | 52,720,317.40 | 67,121,367.95 | 127% |
| **JUMLA UNGUJA** | **1,007,959,612.20** | **380,927,918.88** | **38%** |
| CHAKE CHAKE | 67,315,300.00 | 43,814,601.00 | 65% |
| MKOANI | 44,545,100.60 | 33,102,679.80 | 74% |
| WETE | 37,915,949.90 | 36,096,843.70 | 95% |
| MICHEWENI | 30,000,000.00 | 29,233,356.80 | 97% |
| **JUMLA PEMBA** | **178,776,350.50** | **142,247,481.3** | **79%** |
| **JUMLA KUU** | **1,307,942,627.90** | **523,175,400.18** | **40%** |

## Kiambatisho namba 5

# MAREJESHO YA FEDHA ZA MIKOPO (UNGUJA NA PEMBA)

| S/N | PROGRAMU | IDADI YA MIKOPO | THAMANI YA FEDHA | WALIOPATIWA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | WANAUME | WANAWAKE | JUMLA |
| | | **UNGUJA** | | | | |
| | INUKA | 356 | 3,033,100,000 | 353 | 297 | 650 |
| | Mikopo ya makundi maalum (4.4.2) | 71 | 581,353,000 | 106 | 760 | 866 |
| | Khalifa/ Abudhabi Fund | 15 | 1,274,300,000 | 45 | 31 | 76 |
| | Vifaa vya ufugaji wa Nyuki | 15 | 28,125,000 | 53 | 47 | 100 |
| | **Jumla Unguja** | **457** | **4,916,878,000** | **557** | **1135** | **1692** |
| | | **PEMBA** | | | | |
| | INUKA | 149 | 1,001,783,637.03 | 143 | 70 | 213 |
| | Mikopo ya makundi maalum (4.4.2) | 87 | 697,505,000 | 153 | 603 | 756 |
| | **Jumla Pemba** | **236** | **1,699,288,637.03** | **296** | **673** | **969** |
| | **JUMLA KUU** | **693** | **6,616,166,637.03** | **853** | **1,808** | **2,661** |

## Kiambatisho namba 6

## MAREJESHO YA FEDHA ZA MIKOPO (UNGUJA NA PEMBA)

| PROGRAMU | FEDHA ZILIZOKUSANYWA |
|---|---|
| **UNGUJA** | |
| Inuka | 5,047,368,526.69 |
| Khalifa | 866,150,246.42 |
| Makundi maalum (4.4.2) | 39,462,210.03 |
| Mbogamboga | 1,040,000 |
| Uwezeshaji | 3,374,000 |
| Vifaa vya nyuki | 9,000,000 |
| **Jumla Unguja** | **5,966,394,983.14** |
| **PEMBA** | |
| Inuka | 2,047,957,166.50 |
| Makundi Maalumu | 313,472,222.22 |
| Mbogamboga | 2,063,000. |
| Uwezeshaji | 2,610,000 |
| **Jumla Pemba** | **2,366,102,388.72** |
| **Jumla Kuu** | **8,332,497,371.86** |

**Kiambatisho nambari 7**

## MAFUNZO YALIYOTOLEWA UNGUJA

| AINA YA MAFUNZO | W/ME | W/KE | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Nadharia ya ujasiriamali na umuhimu wake | 242 | 527 | 769 |
| Ufugaji wa nyuki | 56 | 44 | 100 |
| Umeme wa Jua | 0 | 46 | 46 |
| Usarifu wa Matunda na mboga mboga | 40 | 115 | 155 |
| Elimu ya kifedha (ikiwemo uandishi wa mpango wa Biashara na pre-loan) | 205 | 1,385 | 1,590 |
| Masuala ya masoko | 7 | 29 | 36 |
| **Jumla Unguja** | **550** | **2,146** | **2,696** |

## MAFUNZO YALIYOTOLEWA PEMBA.

| AINA YA MAFUNZO | W/ME | W/KE | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Mabadiliko ya Tabia Nchi na Kalenda kwa wajasiriamali. | 31 | 26 | 57 |
| Mafunzo kabla ya kupatiwa mikopo (pre- loan training) | 68 | 103 | 171 |
| Usarifu wa mazao na kuongeza mnyororo wa thamani bidhaa kwa wajasiriamali | 8 | 14 | 22 |
| Mafunzo kuhusu mifumo ya Tenda Serikalini. | 16 | 8 | 24 |
| Mafunzo ya usarifu wa chumvi | 31 | 03 | 34 |
| Mafunzo ya ufugaji kuku | 19 | 27 | 46 |
| Mafunzo ya usarifu wa tomato | 18 | 03 | 21 |
| Mafunzo ya nadharia ya ujasiriamali na kuwaonesha zinazopatikana ZEEA | 09 | 18 | 27 |
| **Jumla Pemba** | **200** | **202** | **402** |

## Kiambatisho nambari. 8

### MAOMBI YA FEDHA 2025/2026 (FUNGU A07)

| PROGRAMU | MATUMIZI YA KAWAIDA | MISHAHARA | RUZUKU YA OC | RUZUKU YA MISHAHARA | MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **PA0702 : Programu kuu ya usimamizi wa viwango vya kazi na upatikanaji wa ajira** | **-** | **-** | **1,358,000,000** | **1,461,300,000** | **-** | **2,819,300,000** |
| SA070201: Programu ndogo ya uratibu wa upatikanaji wa Ajira | | | 384,652,000 | | | **384,652,000** |
| SA070202: Programu ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini | | | 400,746,000 | | | **400,746,000** |
| SA070203: Programu ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi na usuluhishi wa migogoro ya kazi | | | 572,602,000 | 1,461,300,000 | | **2,033,902,000** |
| **PA0703: Programu kuu ya Uimarishaji wa vyama vya Ushirika** | **515,200,000** | **306,243,000** | **-** | | **-** | **821,443,000** |
| SA070302: Programu ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika | 515,200,000 | 306,243,000 | | | | **821,443,000** |

| PROGRAMU | MATUMIZI YA KAWAIDA | MISHAHARA | RUZUKU YA OC | RUZUKU YA MISHAHARA | MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **PA0704: Programu kuu ya Kukuza Uwekezaji Nchini KUKUZA NA KUIMRISHA UWEKEZAJI** | **785,642,000** | **83,703,000** | **-** | **3,911,300,000** | **15,000,000,000** | **19,780,645,000** |
| SA070401: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Uwekezaji Binafsi (ZIPA) | | | | 3,911,300,000 | 15,000,000,000 | **18,911,300,000** |
| SA070402: Programu ndogo ya Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma kupitia ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) | 785,642,000 | 83,703,000 | | | | **869,345,000** |
| **PA0705: Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji** | **3,225,758,000** | **2,053,154,000** | | **-** | | **5,278,912,000** |
| SA070501: Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti | 799,330,000 | 215,284,000 | | | | **1,014,614,000** |
| SA070502: Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji | 1,696,368,000 | 1,331,361,000 | | | | **3,027,729,000** |
| **PROGRAMU** | **MATUMIZI YA KAWAIDA** | **MISHAHARA** | **RUZUKU YA OC** | **RUZUKU YA MISHAHARA** | **MAENDELEO** | **JUMLA** |
| SA070503: Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba | 730,060,000 | 506,509,000 | | | | **1,236,569,000** |
| **JUMLA KUU** | **4,526,600,000** | **2,443,100,000** | **1,358,000,000** | **1,461,300,000** | **-** | **28,700,300,000** |

## Kiambatisho nambari. 9

### MAOMBI YA FEDHA 2025/2026 (FUNGU A11)

| Programu | Matumizi ya kawaida (TZS) | Mishahara (TZS) | Mchango wa SMZ (TZS) | Washirika wa Maendeleo (TZS) | Jumla (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| **PA1101: Programu kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi** | **464,500,000** | **-** | **4,500,000,000** | **6,100,000,000** | **11,064,500,000** |
| SA110101: Programu ndogo ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 464,500,000 | - | 4,500,000,000 | 6,100,000,000 | 11,064,500,000 |
| **PA1102: Programu Kuu ya Utumishi na Uendeshaji wa Taasisi ya ZEEA** | **1,858,700,000** | **1,733,400,000** | **-** | **-** | **3,592,100,000** |
| SA110201: Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji | 1,408,700,000 | 1,472,466,000 | - | - | 2,881,166,000 |
| SA110202:Programu ndogo ya Afisi ya Uratibu - Pemba | 450,000,000 | 260,934,000 | - | - | 710,934,000 |
| **JUMLA KUU** | **2,323,200,000** | **1,733,400,000** | **4,500,000,000** | **6,100,000,000** | **14,656,600,000** |